



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA MBOZI

Simu . Na. 025 – 2580272  
Nukushi Na. 025 – 2580044  
Baruapepe.ded@mbozidc.go.tz

S. L. P. 3,  
MBOZI.

*Unapojibu tafadhali taja:*

**Kumb.Na.A.10/MDC/31/6**

**23 Mei, 2023.**

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mbozi anawatangazia nafasi za kazi za Mtendaji wa Kijiji Daraja la III. Nafasi hizi za ajira zinatokana na kibali cha ajira kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa barua Kumb.Na.FA.170/571/01”A”/47 ya tarehe 17 Februari, 2023. Aidha, tangazo hili linafuta tangazo lenye Kumb.Na.A.10/MDC/31/3 la tarehe 14 Machi, 2023

**1.0. MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III (NAFASI 3)**

**1.1 SIFA ZA MWOMBAJI**

Mwombaji anatakiwa awe na cheti cha kufaulu Kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI) na waliohitimu mafunzo ya Cheti (Astashahada) katika fani zifuatazo: Utawala, Uongozi na Usimamizi wa Fedha, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo au Chuo/Taasisi yoyote inayotambuliwa na Serikali.

**1.2 KAZI NA MAJUKUMU**

- i. Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- ii. Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- iii. Kiongozi wa wataalam (Watumishi wa Serikali) katika Kijiji.
- iv. Mhasibu (Afisa Masuuli) na Mtendaji Mkuu wa kazi za kila siku za Serikali ya Kijiji.
- v. Kutafsiri na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Taratibu zinazotolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- vi. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa raia na mali zao, kuwa Mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- vii. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- viii. Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- ix. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na Mwajiri.

### **1.3 MSHAHARA**

- Mshahara atalipwa kwa kuzingatia viwango vya Serikali TGS B1

### **2.0 MASHARTI YA JUMLA**

- Waombaji wote wawe ni raia wa Tanzania wenye umri kuanzia miaka 18 na wasiozidi miaka 45.
- Mwombaji awasilishe picha moja ya hivi karibuni (Passport size).
- Waombaji wawasilishe maelezo binafsi yanayojitosheleza yenye anuani za namba za simu.
- Waombaji wote waambatanishe nakala ya vyeti halisi vya masomo na taaluma (NTA Level 5) na Transcript ya cheti cha taaluma, cheti cha kuzaliwa. Mwombaji atakayewasilisha "Result" "statement of result", "provisional result" au "Transcript" bila nakala halisi ya cheti cha taaluma maombi yake hayatakubaliwa.
- Kwa waliosoma nje ya nchi Elimu ya Kidato cha nne na Kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
- Waombaji wawasilishe nakala ya kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
- Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoainishwa hayatashughulikiwa.
- Maombi yaandikwe kwa mkono na yatumwe kwa njia ya Posta kupitia anuani iliyotajwa hapo chini.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **29/05/2023**. Aidha, maombi yote yatakayoletwa nje ya Posta hayatapokelewa.

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA MBOZI,  
S.L.P 3,  
MBOZI.**

Imetolewa na.



Abdallah H. Nandonde

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**

**MBOZI.**